SautiElimu

hakielimu

Toleo la 6
2004

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org



Rushwa imekithiri ununuzi wa vifaa vya shule

Wadau wa elimu, Misungwi

Sisi wadau wa elimu wilayani Missungwi tunapenda kuwapongeza walimu kwa juhudi wanazofanya katika kuboresha elimu pamoja na mazingira magumu yanayowazunguka.

Kinachotusikitisha ni kuona kwamba baadhi ya viongozi wa wilaya wanaendekeza vitendo vya rushwa ambavyo vinazorotesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na kukandamiza haki za walimu na kamati za shule.

Katika utekelezaji wa mpango wa MMEM walimu wakuu na wenyekiti wa kamati za shule wamekuwa wakilazimishwa kununua vifaa katika maduka fulani. Inasadikiwa kwamba baadhi ya viongozi ngazi ya wilaya wana hisa katika maduka hayo!

Mathalan, kuna baadhi ya viongozi ambao kazi yao imekuwa ni kuwasaidia walimu kupata hundi haraka kwa ajili ya kuwalipa wazabuni. Viongozi hao baadaye humlazimisha kila mwalimu mkuu awape Tsh. 40,000/- kama 'shukrani' ya kuwasaidia! Mwalimu atakayekataa kufuata maagizo ya viongozi hao hujikuta akiandikiwa barua za kumtishia kufukuzwa kazi.

Tunaiomba Taasisi ya Kuzuia Rushwa (PCB) izunguke wilayani hapa kufuatilia madai haya na kuyafanyia kazi. Bila hivyo, wilaya hii itaendelea kuhujumiwa kielimu!

Tunaandika barua hii kwa uchungu sana.hivi ni sahihi kuwatimizia walimu madai yao ukiwaribia uchaguzi tu? kwanini tujadili na kuwatumia malalamiko wahusika lakini hakuna ufuatiliaji? Tunataka mabadiliko!

Rushwa ni nini?

Na Rakesh Rajani, Mhariri Mkuu

Rushwa ni nini? Kwangu mimi, rushwa inajitokeza katika sura 3:

1. Rushwa ni kuwaibia watu masikini. Watu wengi wanaotoa rushwa ni masikini. Kutoa rushwa inamaanisha kipato chao kitapungua na hawataweza kukidhi mahitaji yao. Mwalimu ambaye atalazimika kutoa rushwa ili apate mshahara wake au mzazi wa kijijini atakayetoa rushwa kupata nafasi ya sekondari atakuwa na upungufu wa chakula, mavazi na dawa.

Wakati mali za umma zinapotumiwa vibaya, kama vile kuiba sementi au kununua vitabu kwa bei ya juu, ina maana watu masikini watapungukiwa. Matajiri wanaweza kujenga madarasa yao na kununua vitabu kwa ajili ya watoto wao; watu masikini hawawezi.

2. Rushwa ni uozo katika uongozi. Palipo na uongozi bora, kiwango cha rushwa kitakuwa kidogo sana. Kwa nini? Kwa sababu viongozi watakuwa karibu na wananchi na kufahamu kila kinachoendelea. Watahisi uchungu wanaoupata masikini na kupambana na rushwa. Hawatatumia madaraka yao vibaya kwa manufaa binafsi.

Barua na ripoti tunazopata zinadokeza kuwa viongozi wengi hawaongozi mapambano dhidi ya rushwa. Badala yake baadhi ya viongozi wenyewe wamegeuka kuwa tatizo. Watu wanaopaswa kututetea wametugeuka na kuanza kutuibia. Hali hii inajidhihirisha katika sehemu nyingi ambapo hata maana ya uongozi imepotea na kuoza.

3. Rushwa inakuza maadili yaliyooza. Tunaambiwa mara kwa mara kwamba mambo muhimu katika maisha ni ukweli, sheria, utu na haki. Hayo ndiyo maadili makuu katika jumuiya yoyote. Lakini katika utendaji tunaona kinyume cha hayo.

Hayo yanapotokea, watu wanajifunza kuwa yote ni maneno matupu, na kwamba maisha ni rushwa, ulaghai, kukosa haki na unyama. Wanafunzi shuleni wanapoona rushwa imetapakaa kila mahali, na hakuna la maana linalofanyika, wanajifunza kwamba rushwa ndiyo njia ya maisha. Mwalimu Nyerere alikuwa akisisitiza kwamba maneno matupu hayavunji mfupa!

Tunapoikubali rushwa, tumehongwa. Nitafanya nini kupambana na rushwa? Na je wewe? Utafanya nini?

Shindano kuhusu rushwa katika elimu

Mwezi Novemba 2003, PCB na HakiElimu walizindua shindano la insha kuhusu kupambana na rushwa katika elimu. Lengo lake lilikuwa ni kubainisha rushwa zinazojitokeza na njia za kupambana na tatizo hilo.

Ushiriki ulikuwa ni mzuri sana. Tulipokea majibu 2,898 kutoka sehemu mbalimbali nchini. Mawazo yote yalikuwa ni muhimu. Michango yote itafanyiwa tathmini na kusambazwa kwa Serikali na kwa jamii. Michango bora pia itatumika kuchapisha kijitabu.

Walipatikana washindi 17 ambao kila mmoja alipata Tsh. 100,000/- kwa ajili yake na nyingine 100,000/- zilipelekwa kwenye shule aliyoichagua (Tazama jedwali hapo chini). Washindi wengine 110 waliofanya vizuri kila mmoja alitumiwa fulana ya PCB.

Jina	Umri	Jinsi	Anapotoka
Leonida J. Kasoga	13	Ke	Tabora
Theresia Gervas	15	Ke	Mwanza
Leah A. Sanga	15	Ke	Dar es Salaam
Twaha Hamisi Ubwa	17	Me	Singida
Mercy Charles Masasi	19	Ke	Dar es Salaam
Hamis Mtingwa	19	Me	Dar es Salaam
Martin P. Mkumbo	19	Me	Dar es Salaam
Beatus Mwendwa	23	Me	Mwanza
Steven D. Kipili	25	Me	Dar es Salaam
Jodos S. Gwemela	31	Me	Tabora
Rajab A Ngimba	32	Me	Ngerengere, Morogoro
Ngikundaeli E. Mghasse	32	Me	Monduli, Arusha
Redempta B. Minga	38	Ke	Mbeya
Norbert N. Mpunga	39	Me	Tandahimba, Mtwara
Ephraim E. Baruti	44	Me	Igunga, Tabora
Padri Michael Kumalija	50	Me	Shinyanga
Gerald W. Ndyamukama	55	Me	Muleba, Kagera

PCB na *HakiElimu* tunawapongeza washindi!

Rushwa ya ngono inawaathiri zaidi wasichana

Na Stellah Mhelela, SLP 253, Mwanza

Kati ya rushwa zinazoongoza katika elimu ni pamoja na rushwa ya ngono. Rushwa hii kwa kiasi kikubwa imekuwa ikimuathiri mwanafunzi wa kike.

Tatizo la wasichana kupata mimba wakiwa shuleni linatokana na rushwa ingawa haichukuliwi hivyo na jamii. Msichana anapopata mimba akiwa shuleni huonekana hafai na kuwa mzigo kwa familia yake. Jamii pia humtenga bila kuchunguza chanzo cha tatizo. Kwa upande mwingine aliyesababisha msichana kupata mimba hawajibishwi. Msichana anadhalilishwa na kuadhibiwa kama mkosefu.

Kuna utata mkubwa katika kufanya maamuzi hasa kwa jinsi adhabu inavyotolewa kwa wahusika. Hadi sasa Serikali imeshindwa kutoa msimamo kuhusu hatma ya msichana anayepata mimba akiwa shuleni. Jambo la kujiuliza ni je, taifa linafaidika vipi kwa kumfukuza shule msichana?

Mara nyingi wasichana wanaoathirika zaidi ni wale wanaotoka katika familia masikini. Wazazi wenye uwezo hutumia mbinu mbalimbali ikiwemo kutoa rushwa ili watoto wao warejeshwe shuleni. Wasichana waliopata mimba shuleni wanaponyimwa nafasi ya kuendelea na masomo tunaongeza idadi ya watu wasio na elimu nchini.

Ni matumaini yangu kwamba Serikali itatunga sheria za kumlinda msichana anayepata mimba akiwa shuleni ili aweze kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imempa msichana, hasa wa kutoka familia masikini, haki ya kupata elimu sawa na watoto wa wenye uwezo.

Jipatie mabango yenye nukuu za Rais Mkapa



HakiElimu imechapisha mabango 5 yenye nukuu za Rais Mkapa kuhusu utawala bora na uwajibikaji. *Marafiki wa Elimu* wote pamoja na wengine tunaowatumia nakala ya *SautiElimu* wamepata seti moja ya mabango yenye nukuu za Rais Mkapa. Iwapo utahitaji tafadhali tuandikie.

Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la 6
2004
ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3• Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Maoni ya washiriki kuhusu rushwa katika elimu

Na Godfrey Telli, *HakiElimu*

Shindano la rushwa katika Elimu limeibua taarifa muhimu.

Rushwa iliyojitokeza zaidi ni ile ya ngono. Ilionekana kutolewa zaidi na wahusika katika jamii kwa wale wenye mamlaka katika mfumo wa elimu kwa sababu mbalimbali.

Mzazi kufanya ngono na mwalimu ili mtoto aandikishwe shule. Mwanafunzi kufanya ngono na mwalimu ili kufaulu mitihani. Mwalimu kufanya ngono na mwalimu mkuu



au Afisa Elimu ili kupanda cheo au kuzuia uhamisho.

Martin Peter Mkumbo anaeleza; "Rushwa ya pesa, ngono pamoja na zawadi mbalimbali zimekuwa zikitolewa na walimu kwa wakubwa zao (maafisa na waratibu wa elimu) ili kupandishwa vyeo, kupewa uhamisho au kufutiwa makosa mbalimbali wanayofanya kama; kutowajibika ipasavyo, kufanya mapenzi na kuwapa ujauzito wanafunzi, nk."

Idadi kubwa ya washiriki waliongelea rushwa ya fedha na zawadi. Rushwa hii imeenea zaidi katika maeneo ya mijini ingawa ipo pia vijijini. Inajitokeza zaidi katika mfumo wa 'tuition', kununua mitihani, kulipiwa karo na katika uandikishwaji wa wanafunzi shuleni.

Kwa upande wa vijijini inatokea kwa kuwafanyisha kazi wanafunzi kwa walimu, viongozi wa elimu na hata viongozi wengine. Kazi hizo ni kama kukata kuni, kuchota maji, kulisha mifugo nk.

Ngikundael E. Mghasse anasema; "Sehemu za mijini wakati wa uandikishwaji shule walimu wakuu husema nafasi zimejaa ili mwombaji atoe kitu kidogo. Lakini sehemu za vijijini hususan katika jamii za wafugaji, watu hutoa mbuzi, ng'ombe, nk., kwa walimu ili watoto wao wasiandikishwe shule."

Wako wengine waliotoa maoni kwamba mishahara na marupurupu ya walimu yaangaliwe upya. Elimu zaidi kwa kutumia vyombo vya habari na madhehebu ya dini pia imeonekana na wengi kama njia muafaka ya kupambana na tatizo la rushwa katika elimu. Wamependekeza adhabu kali zitolewe kwa wale watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mwisho, viongozi kuwa wazi na karibu na wananchi na kuwajibika kwao ni muhimu kama anvyosema Padri Michael Kumalija:"Viongozi pamoja na watumishi mbalimbali wa umma wamewekwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na sio kuwachuna kwa njia ya udanganyifu. Hivyo mnapaswa kuwa karibu na wananchi ili maamuzi pamoja na vitendo vyao wavifanye bila kificho ili wananchi wayaone waziwazi matendo yao na kutambua kinachoendelea."

Nini kifanyike kupambana na rushwa?

Na Razack A. Kijumbe, SLP 4, Kilwa-Masoko

Baadhi ya njia zinazoweza kutumika kupambana na rushwa katika elimu ni kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili waweze kutambua haki zao. Elimu hiyo inaweza kutolewa kwa njia mbalimbali kupitia redioni, midahalo ya wazi katika jamii na ndani ya mikutano ya kamati za shule.

Mbinu nyingine ya kupambana na rushwa ni kuingiza somo la rushwa katika mitaala. Somo la rushwa na madhara yake lifundishwe kuanzia vyuo vya ualimu, shule za msingi hadi elimu ya juu. Kwa hali hiyo walimu na wanafunzi wataanza kuelewa madhara ya rushwa kuanzia awali.

Habari ni nguvu. Hivyo basi wananchi wafuatilie habari kuhusu sera mbalimbali za maendeleo. Mfano katika utekelezaji wa MMEM, wananchi wana haki ya kufahamu hesabu za mapato na matumizi. Hesabu hizo ziwekwe wazi, kwenye mbao za matangazo ili kuondoa utata.

Njia nyingine ni kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza umaskini kote nchini. Umaskini na ufinyu wa kipato vinasababisha watu kushawishika kutoa au kupokea rushwa. Uwazi na uwajibikaji wa viongozi katika kuwatumikia wananchi pia utapunguza au kuondoa rushwa.

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala na midahalo ya umma, kufanya utafiti yakinifu, weriye kuhoji, kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

ISSN 08568588

© HakiElimu, 2004

Mhariri Mkuu: Rakesh Rajani
Timu ya *SautiElimu*: Lilian R. Kallaghe, Wema Msigwa na Godfrey Telli
Mchoraji: Hamisi Mtingwa

Tuandikie!

HakiElimu, *SautiElimu*
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: 022 2151852 / 3
Fax: 022 2152449
Barua Pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org



Ukurasa wa 2

Barua kwa *SautiElimu*

Pongezi PCB kwa shindano la rushwa
Ili kupambana na rushwa katika elimu ni muhimu kwanza; Mwalimu apate haki zake zote bila kusumbuliwa. Hii itamwezesha kuepuka vishawishi vya rushwa na kuzingatia maadili yake ya kazi.



Kwa upande wa wanafunzi ni muhimu wapate elimu bora itakayowawezesha kujua haki zao za msingi ili wasishawishike kutoa wala kupokea rushwa.

Mwisho, nawapongeza Taasisi ya Kuzuia Rushwa (PCB) kwa shindano la Rushwa katika Elimu. Shindano hilo limesaidia kuwaamsha wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla juu ya matatizo ya rushwa yanayoshamiri katika jamii. Vilevile shindano limetoa changamoto ya namna ya kukabiliana na rushwa.

Mollen Masaka
Shule ya Msingi Itigi
SLP 30
Itigi-Manyoni

• • •

Rushwa ya ngono inaathiri elimu
Rushwa ya mapenzi ni moja ya rushwa mbaya sana ambayo inazidi kushamiri katika elimu. Walimu au wanafunzi hutumia rushwa hii kuweza kufanikisha matakwa yao.

Imekuwa jambo la kawaida kwa walimu wa jinsia zote kuwarubuni wanafunzi kutoa rushwa ya ngono. Rushwa hii hutolewa kwa ahadi ya kuwapa majibu ya mitihani au alama za juu katika masomo na hasa wakati wa mitihani.

Kwa upande mwingine wanafunzi hasa vyuoni, nao huwashawishi walimu na kuomba msaada wa kielimu huku wakiwaahidi rushwa ya ngono. Kutokana na udhaifu wa kibinadamu, walimu nao hujikuta wameingia katika mtego wa kutembea na wanafunzi wao.

Rushwa hii inaathiri elimu nchini kwani hapo baadaye taifa litakuwa na wahitimu wengi wasio na ujuzi. Rushwa ya ngono ni hatari kwani huweza kusambaza virusi vya UKIMWI. Pia itasababisha kupoteza maisha ya walimu na wanafunzi ambao wanategemewa sana na jamii.

Glory E. Mponzi
SLP 32038
Dar es Salaam

• • •

Ufujaji mali za shule ni rushwa!
Matumizi mabaya ya pesa na mali za shule ambayo hufanywa na baadhi ya walimu ni aina moja ya rushwa inayochangia kurudisha nyuma maendeleo ya elimu nchini. Walimu hao na viongozi wengine wa shule hutumia vibaya nafasi walizonazo kuziibia shule na kufuja mali kwa manufaa yao binafsi. Nashauri uongozi wa elimu katika ngazi zote kufanya ukaguzi wa mali za shule mara kwa mara.

Urasimu uliopo katika ofisi mbalimbali za umma na idara za elimu pia husababisha mianya ya rushwa. Baadhi ya watendaji katika taasisi za elimu wamekuwa wakikwamisha kazi kama vile kushughulikia maslahi na malalamiko ya walimu na wanafunzi kwa makusudi ili wapewe rushwa.

Umaskini katika jamii pia ni moja ya sababu kuu inayochangia kuongezeka kwa rushwa. Wadau wengi wa elimu na hasa walimu wamejikuta wakitoa ama kupokea rushwa kutokana na hali ngumu ya maisha. Nashauri wabunge wawe karibu na wananchi ili kuwawezesha kupata habari na kufahamu kwamba hawastahili kulipia haki zao.

Chrispin Mukerebe
SLP 9074
Dar es Salaam

Elimu ya rushwa imlenge mtoaji, mpokeaji
Napenda kutoa maoni yangu kwamba rushwa katika elimu inatolewa kwa kuanzia na mwanafunzi hadi maafisa wa ngazi za juu katika idara ya elimu.

Wanafunzi hutoa rushwa kwa njia nyingi ikiwemo kufanya kazi kwa walimu kama vile kufua nguo, kulima, kuchota maji, kuuza bidhaa mbalimbali na hata kulea watoto ili wapate alama nzuri zitakazowawezesha kushinda mitihani.

Wazazi nao wanashiriki katika kutoa rushwa wakati wa kuandikisha watoto shule, kuhamisha wanafunzi, kupatiwa majibu ya mitihani na hata kuchaguliwa kuendelea na elimu ya juu.

Baadhi ya watendaji wengine wa Wizara ya Elimu wanahusika na rushwa kwa kudai chochote wakati wa kushughulikia matatizo ya wazazi na walimu kama vile kupanda vyeo na uhamisho, kwa wakaguzi wa miradi mbalimbali, kamati za shule na kupandishwa madaraja.

Nashauri elimu ya rushwa kwa umma itolewe kwa kumlenga mtoaji na mpokeaji. Serikali iongeze nafasi za shule kuanzia msingi hadi sekondari. Pia maslahi ya walimu na watendaji katika idara mbalimbali za elimu yaboreshwe ili kuepuka tamaa ya kupokea au kutoa rushwa.

Mary I. Maufi
SLP 172
Mpanda-Tabora

• • •

Tuition kichocheo cha rushwa
Rushwa inawagawa watoto kulingana na uwezo wa wazazi wao kifedha. Utakuta watoto wenye uwezo wanafundishwa masomo ya ziada (tuition) na kuwabagua watoto wa masikini. Kwa sababu ya kupokea fedha, walimu hufundisha kidogo darasani na kutumia muda na nguvu zao nyingi kufundisha tuition watoto walio na uwezo.

Rushwa katika sekta ya elimu husababisha walimu wa jinsi moja kurundikana katika shule moja kwa kisingizio cha kuwafuata wanandoa wenzao. Hii inasababisha baadhi ya shule kuwa na walimu wengi wakati nyingine hazina walimu kabisa, hasa za vijijini.

Ushauri wangu ni kwamba majina ya walimu wanaofuata maadili na wenye nidhamu kazini yapendekezwe na kamati za shule wizarani ili wapewe motisha, kupandishwa vyeo na kupewa nafasi za masomo bila usumbufu.

Zainabu Ramadhani
SLP 28
Kibiti-Rufiji

• • •

Watendaji Elimu wahamishwe mara kwa mara
Baadhi ya njia zinazoweza kutumika kupambana na rushwa katika elimu ni kubadilishwa mara kwa mara kwa uongozi wa elimu ngazi ya wilaya. Hii itaepusha viongozi kuzoeana sana na walimu na hivyo kushawishika kupokea rushwa.

Mfano, katika idara za elimu, rushwa hutolewa na baadhi ya walimu kwa makarani au wahudumu waliowazoea ili waweze kupeleka mafaili ya wahusika kwenye ofisi za maafisa wa ngazi za juu kwa ajili ya kutolewa maamuzi.

Napendekeza pia kuwe na maafisa ukaguzi watakaoshughulikia maslahi ya walimu wilayani. Ukaguzi ufanyike mara kwa mara ili kuona kama madai ya walimu yanatimizwa bila vikwazo na kwa wakati muafaka.

Sophia G. Range
SLP 71 ADEM
Bagamoyo-Pwani



Je, una taarifa zozote za Rushwa?
Waandikie PCB wilayani kwako au tuma barua kwa PCB, SLP 9865, Dar es Salaam